

Aonya wanaotumia misikiti, kanisa kusaka urais

■ Nora Damian

MWENYEKITI wa Taasisi ya Kiislamu ya Imam Bukhary, Sheikh Khalifa Khamis, amewataka Watanzania kujiepusha na hatari ya kuikabidhi nchi kwa mafisadi, kwani baadhi ya watu wamekuwa wakipita kwenye nyumba za ibada na kumwaga fedha kwa lengo la kupata uongozi.

Akizungumza kwenye semina kuhusu wajibu wa viongozi wa dini kwa jamii jana, Sheikh Khalifa alisema wananchi wanatakiwa kung'amua watu hao wanahangaika kwenye nyumba za ibada kusaka madaraka.

Alisema hivi sasa siyo wakati wa kampeni, kwani uchaguzi ume-shapita hivyo watu wanatakiwa kufanya kazi ili nchi ipate maendeleo na waondokane na umasikini. Pia, aliwataka Waislamu kujitokeza kutoa pindi tume ya kukusanya maoni ya kuunda katiba mpya itakapoundwa.

Alisema katiba ni mkataba baina ya watalawa na wananchi, hivyo watu wote wanatakiwa watumie nafasi zao vizuri ili maoni yao yaweze kuingizwa kwenye katiba mpya.

Naye Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum, amewataka Waislamu kuwapuza watu wanaowashawishi

wasishiriki kwenye mchakato wa uundaji Katiba Mpya.

Ijumaa iliyopita, baadhi ya watu wasiojulikana walisambaza vipeperushi kwenye misikiti mbalimbali, vikiwa na ujumbe wa kuwataka Waislamu wasishiriki kwenye mchakato wa uundaji katiba. "Hawa wanaosambaza vipeperushi misikitini tutawapiga vita, wanataka kuturudisha nyuma tuwapuuzwa kwa sababu kila mtu ana haki ya kushiriki," alisema Alhad.

Pia, Alhadi alisema wanajipanga kuona yale yanayowahusu yanachukua nafasi katika katiba mpya na kuwataka Waislamu kujiandaa kutoa maoni yao.